

**HOTUBA YA BI. FAUSTA MUSOKWA, MKURUGENZI MTENDAJI WA MPITO,
WAKFU WA VYOMBO VYA HABARI - TANZANIA MEDIA FOUNDATION (TMF)
KATIKA SIKU YA MAADHIMISHO YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI
DUNIANI, TAREHE 3 MEI, 2018, MORENO, DODOMA.**

MADA: Wajibu wa serikali: Vyombo vya habari, haki na utawala wa sheria.

Ndugu Mgeni Rasmi Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo,

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe Binilith Mahenge,

Mwakilishi Mkazi wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Shirika la Kimataifa la Sayansi na Teknologia (UNESCO), Bi. Anna Therese Ndong Jatta

Mwenyekiti wa MISATAN, Bi Salome Kitomari

Wakurugenzi wa asasi za kiraia na wadau wa Kamati ya Maandalizi ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani,

Wageni waalikukwa,

Waandishi wa habari na wadau wahabari,

Itifaki imezingatiwa.

Habari za asubuhi mabibi na mabwana.

Wakfu wa vyombo vya habari Tanzania -Tanzania Media Foundation (TMF) inayo furaha kuungana na wadau wa habari na wanahabari wote duniani kusherekeea mafanikio, kutathmini maendeleo, kujadili changamoto na kupanga mikakati ya pamoja ili kufikia tasnia ya habari huru na imara. Katika siku hii ya kuadhimisha uhuru wa vyombo vya habari duniani, TMF ingependa kuwapongeza waandishi na wanahabari kwa kazi wanayoifanya kutuhabarisha sisi sote.

Mwaka huu, kauli mbiu ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani ni: **WAJIBU WA SERIKALI: VYOMBO VYA HABARI, HAKI NA UTAWALA WA SHERIA.**

Tasnia ya habari, vyombo vya habari na waandishi wa habari wana nafasi ya kipekee katika kuchochea maendeleo ya nchi. Nafasi yao ni ya kutuwajibisha sisi sote ili tufikie malengo ya maendeleo tuliojiwekea kama nchi kwa kufanya kazi yao kwa weledi, maadili na umakini, bila uoga. Kazi ya sekta ya habari ni kutafuta na kuchambua taarifa ili kutengeneza na kutoa habari kwani upatikanaji wa habari sahihi kwawakati ni daraja litakalo tufikisha kwenye maendeleo.

If information is power then the media are agents of our liberation, for through their work, they empower us.

Kama tunathamini maendeleo, lazima pia tuithamini sekta ya habari kwani ndiyo inayofanya kazi kutuonesha kinachoendelea katika jamii zetu, nchi yetu na dunia kwa ujumla ili tuchukue hatua madhubuti, hasa pale ambapo kuna ukosevu.

Tutaonekana kuthamini maendeleo pale tu ambapo tutaimarisha sekta ya habari na kuiwezesha kufanya kazi yake.

Ili kuimarisha tasnia ya habari, TMF imekuwa ikitoa ruzuku na mafunzo kwa waandishi na vyombo vya habari tangu mwaka 2008, ikiwa kama mradi na baadae kama shirika la kujitegemea. Katika kipindi hiki cha takriban miaka 10, tumetoa ruzuku zaidi ya 900 (count is at least 912) za mawandishi moja moja na 157 kwa taasisi. Ruzuku hizi zimelenga hasa kuibua habari kutoka vijini au kwenye jamii zilizopo pembezoni na kuimarisha mifumo na taratibu za kibiashara katika vyombo vya habari kwaajili ya uendelevu wake na uendelevu wa habari za uchunguzi na za maslahi ya umma.

Kupitia kazi za waandishi na vyombo vya habari vilivyo pata ruzuku na mafunzo kutoka TMF tuna mifano zaidi ya themanini kuhusu namna ambavyo vyombo vya habari vinaweza kuchangia maendeleo ya nchi. Ni dhahiri kwamba waandishi wanapowezeshwa kitaaluma na kifedha, wakiheshimiwa na kulindwa na kuoneshwa ushirikiano, wanaandika habari za kweli na zinazozingatia maslahi ya umma. Pale wanapotimiza wajibu wao kwa namna hii, hatuna budi kuwaunga mkono kama wanajamii na viongozi kwa kufanya kazi changamoto wanazoibua.

Mhe. Mgeni rasmi na washirika wote wa mkutano huu,

Ningekuwa na nafasi na idhini ya waandaaji ningeomba sisi sote tufunge macho, tuzibe masikio na kufunga mikono yetu nyuma ya migongo yetu, kisha tuanze kutembea katika ukumbi huu kila mmoja akiwa na lengo la kufika upande mwingine wa ukumbi kutoka pale alipo. Bila shaka ndani ya muda mfupi kungekuwa na kelele na vurugu za kila aina, watu wakigongana, wakijikwa na wakiumizana. Hivi ndivyo ilivyo jamii inanyokosa mwongozo wa tasnia ya habari iliyo huru na imara.

Tusifike hapo.

Leo, tunapoadhimisha siku hii ya uhuru wa vyombo vya habari duniani tuijulize ni kwa kiasi gani kila muhimili unachangia kuhakikisha kauli mbiu hii ya **WAJIBU WA SERIKALI: VYOMBO VYA HABARI, HAKI NA UTAWALA WA SHERIA** inazingatiwa katika kutoa na kupokea habari.

Tuamue sasa kuongeza kasi na nguvu tunayoiwekeza kwenye kuimarisha tasnia ya habari kwani ni daraja ya kufikia maendeleo tunayoyataka.

ASANTENI SANA.